

## *LENGO LA FALCON KWA KUFAULU!* PBIS Maelezo ya Mzazi

Ikiwa ungependa habari zaidi, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako kwa simu, barua pepe, au binafsi.

Shule ya Msingi ya Alexander

**3571 Sycamore St. SE**  
**Iowa City, IA 52341**  
**(319)688-1095**



Katika Alexander Elementary, sisi hujenga mazingira mazuri ya shule ambapo wanafunzi wote wana mafanikio. Kama vile wanafunzi wote hupata kufundishwa katika kusoma na hesabu, watoto wote katika Alexander hupokea maelekezo katika mfumo wetu wa kiwango cha juu na matarajio wazi ya tabia. Wanafunzi na wanfanya kazi wanashiriki katika mfumo huu. Hii inaitwa **Tier 1 Hatua Chanya ya Tabia na Usaidizi (PBIS)** ama **PBIS ya Shule Yote**.

Tunafundisha tabia nne za **Lengo la Falcon: Uheshimu, Wajibu, Uhusiano, na Utukufu.**

## Nitaona nini katika shule ya mtoto wangu?

### Lengo la kufundisha na kuimarisha tabia zinazo tarajiwa.

- Mabango karibu na jengo na darasani ikieleza tabia zinazo tarajiwa kwa maneno na picha.
- Vipande vidogo vya karatasi vinavyoitwa "Tiketi za Talon" ambazo hupewa wanafunzi kwa kifikia matarajio na kubadilishana kwa pendeleo la mwanafunzi na tuzo katika kila darasa.
- Maadhimisho ya mwezi ya shule ikiwa ni pamoja na makusanyiko ya wanafunzi, usiku wa familia, michezo, nk.

### Lengo la kuzuia tabia za tatizo na kutabiri matokeo wakati zinatokea.

- Katika kila mwaka wafanyakazi wa shule hutoa mafundisho na taratibu na kufanya mazoezi na wanafunzi.
- Wafanyakazi kwa wazi hueleza tabia zinasotarajiwa na matokeo yaliyotarajiwa kwa tabia nzuri au mbaya. Unaweza kusikia maneno kama tabia ya "Juu ya Mstari na Chini ya Mstari".
- Kila darasani imepanga sehemu ya wanafunzi kupata lengo na kutafakari.

### Mawasiliano mara kwa mara na ushirikiano kati ya familia na walimu kuhusu mafanikio ya mwanafunzi na mahitaji.

- Majarida ya darasani, ujumbe wa maandishi, simu, na barua pepe.
- Mikutano ya kibinafsi kati ya familia na shule.
- Ziara na shughuli za nyumbani na jamii.

## Kutakuwaje ikiwa mtoto wangu anahitaji usaidizi zaidi??

Waalimu na wafanyakazi wa shule hufuatilia mara kwa mara mahitaji ya mwanafunzi na kufanya mapendekezo kwa maagizo maalum zaidi au usaidizi wa kipekee kwa kila mtoto. Wazazi daima hujumuishwa katika majadiliano ya mapendekezo yoyote maalum kwa watoto wao. Wazazi wanaweza pia kuomba msaada wa ziada wakati wowote wanazungumza moja kwa moja na mwalimu wa mtoto wao.

Mpango hii zaidi ya PBIS huitwa **Tier 2 PBIS**. Tier 2 PBIS hutoa majibu ya haraka, ufanisi zaidi, maalum, ya lengo kamili ya kijamii-kihisia na tabia ya kujifunza kwa mtoto wako. **Tier 3 PBIS** hutoa hatua ya kibinasi na ya kiwango cha juu zaidi kwa wale wanafunzi ambao wanaweza kuhitaji mafunzo inayoendelea kuhusu ujuzi wa kijamii-kihisia na tabia katika mfumo wa jumla wa mbinu za shule. Mchoro unaofuata unaonyesha mbinu ya PBIS ya ngazi mbalimbali inayotolewa kwa wanafunzi wote wa Alexander.

